# Ofisi ya Taifa ya Takwimu

S. L. P 796 Simu: 255- (022) 2122722/3/4 Nukushi:+225 (022)2130852
Dar es Salaam,-TANZANIA Barua pepe: dg@nbs.go.tz


*Unapojibu tafadhali taja:*
Kumb Na: NBS/S.40/21/472

**YALIYOJITOKEZA**

Tarehe: 15 Januari, 2013

## FAHIRISI ZA BEI ZA TAIFA MWEZI DESEMBA, 2012

### Utangulizi

### Maana ya Fahirisi za Bei za Taifa

Fahirisi za bei za Taifa ni kipimo kinachotumika kupima mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma mbalimbali zinazotumiwa na jamii. Bei za bidhaa na huduma zipatazo 224 hukusanywa kila mwezi kwa kila mkoa nchini.

### Mizania mpya za bidhaa na huduma za jamii na kizio cha bei

Mizania ya Fahirisi za bei za Taifa zimetokana na matumizi ya kaya binafsi kutoka mikoa 21 ya Tanzania Bara. Mizania inajumuisha matumizi ya kaya zote binafsi kutoka mijini na vijijini. Kizio cha Fahirisi za Bei za Taifa kimebadilishwa kutoka Desemba 2001=100 hadi Septemba 2010=100.

### Makundi ya bidhaa na huduma za jamii

Marejeo ya Fahirisi za Bei za Taifa yamefanyika kwa kufuata makundi yaliyokubalika Kimataifa yanayoitwa mchanganuo wa matumizi binafsi "Classification of Individual Consumption by Purpose (COICOP)". Fahirisi mpya za Bei inajumuisha makundi 12 ya mfumo wa COICOP pamoja na fahirisi za bei kwa makundi maalumu. Makundi hayo maalumu ni; 1) Vyakula na vinywaji baridi—vikijumuisha vyakula vinavyoliwa majumbani na mahotelini; 2) Nishati na Mafuta - kundi hili linajumuisha umeme na aina nyingine za nishati zinazotumika majumbani pamoja na petroli na dizeli; 3) Fahirisi za bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula na vinywaji baridi; 4) Fahirisi za huduma zote za jamii isipokuwa vyakula, vinywaji baridi, nishati na mafuta.

### Namna ya kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa

Maboresho yamefanyika kwenye ukokotoaji wa Fahirisi mpya za Bei za Taifa, ikiwa ni pamoja na kutumia wastani wa jiometria "geometric means" kwenye kukokotoa Fahirisi za Bei katika ngazi za mwanzo badala ya wastani wa kawaida "arithmetic mean", matumizi ya mfumo ulioboreshwa wa ukokotoaji pamoja na mfumo mzima wa kukusanya na kuchambua bei. Kanuni ya "modified Laspeyres index" inaendelea kutumika kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa katika ngazi ya makundi makubwa.

## MFUMUKO WA BEI KWA KIPIMO CHA MWAKA UMEBAKI KUWA ASILIMIA 12.1

### Jedwali Namba 1: Badiliko la Fahirisi za Bei za Taifa kwa Mwezi Desemba, 2012 (Septemba, 2010 = 100)

| Na. | KUNDI (MAIN GROUP) | Mizania (Weight) | Des-2011 | Nov-2012 | Des-2012 | Badiliko la mwezi mmoja | Badiliko la miezi 12 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Vyakula na vinywaji baridi | 47.8 | 131.09 | 143.77 | 148.23 | 3.1 | 13.1 |
| 2 | Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku | 3.3 | 106.59 | 128.30 | 130.89 | 2.0 | 22.8 |
| 3 | Mavazi ya nguo na viatu | 6.7 | 112.96 | 125.12 | 126.02 | 0.7 | 11.6 |
| 4 | Nishati, Maji na Makazi | 9.2 | 122.64 | 142.92 | 143.59 | 0.5 | 17.1 |
| 5 | Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba | 6.7 | 116.10 | 124.99 | 125.65 | 0.5 | 8.2 |
| 6 | Gharama za Afya | 0.9 | 103.38 | 106.29 | 106.87 | 0.5 | 3.4 |
| 7 | Usafirishaji | 9.5 | 112.34 | 115.22 | 115.97 | 0.6 | 3.2 |
| 8 | Mawasiliano | 2.1 | 98.14 | 96.52 | 96.28 | -0.3 | -1.9 |
| 9 | Utamaduni na Burudani | 1.3 | 101.13 | 112.11 | 111.78 | -0.3 | 10.5 |
| 10 | Elimu | 1.7 | 105.79 | 110.75 | 110.75 | 0.0 | 4.7 |
| 11 | Hoteli na Migahawa | 6.4 | 113.99 | 131.19 | 131.90 | 0.5 | 15.7 |
| 12 | Bidhaa na huduma nyinginezo | 4.5 | 108.60 | 116.35 | 118.48 | 1.8 | 9.1 |
| **JUMLA – FAHIRISI BIDHAA ZOTE** | | **100.0** | **121.79** | **133.87** | **136.48** | **1.9** | **12.1** |
| **Makundi Mengine Teule** | | | | | | | |
| 1 | Vyakula—vikijumuisha vyakula vilivyoliwa majumbani na mahotelini | 51.0 | 129.20 | 142.39 | 146.44 | 2.8 | 13.3 |
| 2 | Nishati na Mafuta—kundi hili linajumuisha umeme na aina nyingine za nishati zinazotumika majumbani pamoja na petroli na dizeli | 5.7 | 134.25 | 157.87 | 158.12 | 0.2 | 17.8 |
| 3 | Fahirisi za bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula na vinywaji baridi | 49.0 | 113.03 | 123.78 | 124.69 | 0.7 | 10.3 |
| 4 | Fahirisi na huduma zote za jamii Isipokuwa vyakula, nishati na mafuta | 43.3 | 109.84 | 118.66 | 119.66 | 0.8 | 8.9 |

Mfumuko wa Bei wa Taifa kwa kipimo cha mwaka unapima kiwango cha badiliko la kasi ya bei za bidhaa na huduma zote zinazotumiwa na kaya binafsi. Jedwali namba 1 hapo juu linaonyesha kwamba, Mfumuko wa Bei wa Taifa kwa mwezi Desemba, 2012 umebakia kuwa asilimia 12.1 kama ilivyokuwa mwezi Novemba, 2012. Mfumuko wa Bei wa mwezi Desemba, 2012 unamaanisha kuwa, kasi ya upandaji wa bei za bidhaa na huduma kwa mwezi Desemba, 2012 imekuwa sawa na kasi ya kupanda kwa bei kwa mwezi Novemba, 2012. Hata hivyo, kwa ujumla Fahirisi za Bei zimeongezeka hadi 136.48 mwezi wa Desemba, 2012 kutoka 121.79 mwezi wa Desemba, 2011. Mfumuko wa Bei wa Vyakula na Vinywaji Baridi umepungua hadi kufikia asilimia 13.1 mwezi wa Desemba, 2012 kutoka asilimia 13.4 kwa mwezi wa Novemba, 2012.

### Mfumuko wa Bei kwa Bidhaa za Vyakula na Bidhaa Zisizo za Vyakula


Badiliko la Fahirisi ya Bei za bidhaa za vyakula majumbani na migahawani limepungua hadi asilimia 13.3 mwezi wa Desemba, 2012 ikilinganishwa na asilimia 13.7 mwezi wa Novemba, 2012. Kwa upande mwingine, kasi ya ongezeko la bei kwa bidhaa zisizo za vyakula imeongezeka hadi asilimia 10.3 kwa mwezi wa Desemba, 2012 kutoka asilimia 10.1 mwezi Novemba, 2012.

## Mfumuko wa Bei wa Bidhaa na Huduma Zote Isipokuwa Bidhaa za Vyakula na Nishati

Aina hii ya Fahirisi haijumuishi vyakula vilivyoliwa majumbani na migahawani, vinywaji baridi, petroli, dizeli, gesi ya kupikia, mafuta ya taa, mkaa na umeme. Vyakula na nishati vina sifa ya kuwa na bei ambazo hubadilika mara kwa mara hivyo vikiondolewa kwenye Fahirisi ya bidhaa na huduma zote hubakia Fahirisi ambayo ina mwelekeo imara kwa Watunga Sera.

Mfumuko wa Bei ambao haujumuishi vyakula na nishati kwa mwezi wa Desemba, 2012 umeongezeka hadi asilimia 8.9 ikilinganishwa na asilimia 8.5 mwezi Novemba, 2012. Kwa upande mwingine, Mfumuko wa Bei wa Nishati kwa mwezi Desemba, 2012 umepungua hadi kufikia asilimia 17.8 ikilinganishwa na asilimia 18.6 mwezi wa Novemba, 2012.

### Kielelezo Namba 1: Mwelekeo wa Fahirisi za Bei za Taifa na Mfumuko wa Bei Kutoka Desemba, 2011 Hadi Desemba, 2012. (Septemba 2010 = 100)




Kielelezo Namba 1 hapo juu kinaonyesha kuwa, katika kipindi cha kati ya mwezi Desemba, 2011 hadi Desemba, 2012, kumekuwa na mwenendo wa kuongezeka kwa bei za bidhaa na huduma mbalimbali kama inavyoonyeshwa na Fahirisi za bei. Mfumuko wa Bei umekuwa na mwenendo wa kushuka kutoka asilimia 19.8 mwezi Desemba, 2011 hadi kufikia asilimia 12.1 mwezi Desemba, 2012.

## MFUMUKO WA BEI KWA KIPIMO CHA MWEZI UMEONGEZEKA KWA ASILIMIA 1.9

Mfumuko wa Bei wa mwezi Desemba, 2012 umeongezeka kwa asilimia 1.9 ikilinganishwa na asilimia 0.7 kwa mwezi Novemba, 2012. Fahirisi za Bei zimeongezeka hadi 136.48 mwezi Desemba, 2012 kutoka 133.87 mwezi Novemba, 2012. Kuongezeka kwa Mfumuko wa Bei kumechangiwa na kuongezeka kwa bei za bidhaa za vyakula na zisizo za vyakula. Baadhi ya bidhaa za vyakula zilizo changia kuongezeka kwa mfumuko wa bei ni pamoja na mchele kwa asilimia 6.4, mahindi kwa asilimia 16.8, unga wa mahindi kwa asilimia 14.6, mafuta ya kupikia kwa asilimia 2.5, nyama kwa asilimia 1.8, maziwa kwa asillimia 1.7, machungwa kwa asilimia 3.6, limau kwa asilimia 6.3, papai kwa asilimia 3.7, ndizi za kupikwa kwa asilimia 7.0 na mbogamboga kwa asilimia 3.6. Bidhaa zisizo za vyakula zilizochangia kuongezeka kwa mfumuko wa bei kwa kipimo cha mwezi ni; mavazi kwa asilimia 0.7, viatu kwa asilimia 0.8, mazulia kwa asilimia 1.4,

vifaa vya nyumbani kwa asilimia 1.1, dizeli kwa asilimia 0.8, petroli kwa asilimia 3.0, malazi kwa asilimia 1.8, usafi wa nywele kwa asilimia 3.3 na gharama ya kusaga nafaka kwa asilimia 3.2.


## Thamani ya Shilingi ya Tanzania Mwezi Septemba, 2010 Ikilinganishwa na Mwezi Desemba, 2012

Tafsiri: Thamani ya Shilingi ya Tanzania inapima badiliko la uwezo wa Shilingi ya Tanzania katika kununua bidhaa na huduma zilezile za mlaji ambazo Shilingi ya Tanzania itaweza kununua katika vipindi tofauti. Ikiwa wastani wa Fahirisi za Bei za Taifa unaongezeka, thamani ya fedha hupungua.

Thamani ya shilingi 100 imeendelea kupungua hadi kufikia Shilingi 73 na senti 27 kutoka mwezi Septemba, 2010 hadi Desemba 2012

## MIENENDO YA BEI


### Kielelezo Namba 2: Mienendo ya Bei kwa Makundi Mbalimbali ya Fahirisi za Bei Kutoka Desemba, 2011 Hadi Desemba, 2012. (Septemba 2010 = 100)




Kielelezo Namba 2 hapo juu kinaonyesha mienendo ya bei kwa makundi mbalimbali ya fahirisi za bei kuanzia mwezi Desemba, 2011 hadi mwezi Desemba, 2012. Kwa wastani, Fahirisi za vyakula na vinywaji baridi na Fahirisi za nishati na mafuta zimekuwa na mwenendo wa juu kwa kipindi chote zikilinganishwa na fahirisi zingine. Kundi la nishati na mafuta limeonyesha pia kuwa na mwenendo wa fahirisi usio imara ikilinganishwa na makundi mengine kwa kipindi husika. Fahirisi za bidhaa zisizo za chakula na fahirisi za bidhaa zisizo za chakula pamoja na nishati zimeonyesha mwenendo wa bei ulio imara.

## WASTANI WA MFUMUKO WA BEI KWA MWAKA 2012

**Kielelezo 3: Badiliko la Mfumuko wa Bei wa Taifa kwa Kipimo cha Mwezi Kutoka Mwezi Januari hadi Desemba, 2012. (Septemba 2010 = 100)**




Wastani wa Fahirisi za Bei za Taifa kwa kipindi cha miezi 12 kutoka mwezi Januari hadi Desemba, 2012 zimeongezeka hadi kufikia 130.56 kutoka 112.55 kwa mwaka 2011. Wastani wa Mfumuko wa Bei wa Taifa umeongezeka hadi kufikia asilimia 16.0 mwaka 2012 kutoka asilimia 12.7 kwa mwaka 2011; hili ni ongezeko la asilimia 3.3. Kwa wastani badiliko la Mfumuko wa Bei kwa kipimo cha mwezi umeongezeka kwa asilimia 1.0 kutoka Januari hadi Desemba, 2012 kama inavyoonyeshwa kwenye kielelezo namba 3 hapo juu.


**Mawasiliano: Mkurugenzi Mkuu,**
**Ofisi ya Taifa ya Takwimu**